KATIKA MAHKAMA KUU ZANZIBAR

IMESIKILIZWA TUNGUU

RUFAA YA MADAI NAM. 65 YA 2021

(KUTOKA RUFAA YA MADAI NAM. 5 YA KADHI WA RUFAA NA KUTOKA KESI YA MADAI NAM. 477 YA KADHI WA WILAYA MWANAKWEREKWE)

1. HASSAN FATIH MOHAMED … WAKATA RUFAA
2. SALAMA FATIH MOHAMED

DHIDI YA

1. SALMA MUSSA MACHANO …WAPINGA RUFAA
2. KATIBU MTENDAJI KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

HUKUMU

TAREHE YA UAMUZI: 26.1.2023

MBELE YA: MHESH. ISSA, A. A., J

SHEIKH SAMEER ZULFIKAR

SHEIKH SALEH HAKIM

SHEIKH JUMA FAKIH

SHEIKH KANI MKANGA

Hukumu hii inahusiana na rufaa iliyowasilishwa Mahkamani na kupewa namba 65 ya mwaka 2021. Rufaa hii iliwasilishwa na Hassan Fatih Mohammed na Salama Fatih Mohammed dhidi ya Salma Mussa Machano na Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Rufaa hii inapinga uamuzi uliotolewa na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa chini ya Naibu Kadhi Mkuu Sk. Hassan Othman Ngwali.

Kwa ufupi rufaa hii inatokana na kesi ya Madai Nam. 477 ya 2020 iliyoanzia katika Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe ambayo ilisikilizwa na Sk. Othman

Ame Chum. Mdai katika kesi hiyo ni Hassan Fatih Mohammed na Salama Fatih Mohammed (Wakata rufaa) dhidi ya Salma Mussa Machano na Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana (Wapinga rufaa). Madai katika kesi hiyo kwa mujibu wa hati ya madai ni mirathi ya marehemu Omar Hassan Fatih ambae ameacha shamba moja liliopo Fuoni Kipungani katika mkoa wa Mjini Magharibi.

Mahusiano ya Wakata rufaa na Omar Hassan Fatih ni watoto wa baba mkubwa na mdogo. Marehemu Omar Hassan Fatih alizaa mtoto mmoja anaeitwa Salum Omar Hassan ambae tayari ameshafariki, na Salum Omar Hassan nae amezaa watoto wawili ambao ni Halima Salum Omar na Mwinjuma Salum Omar. Halima tayari ameshafariki lakini anao watoto ambao amewaacha. Mpinga rufaa nam. 1 Salma Mussa Machano alikuwa ni mke wa Salum Omar Hassan na ni mama wa Halima Salum Omar.

Wakata rufaa wao wanadai kwamba Salum Omar Hassan alikuwa ni mtoto wa nje ya ndoa, hivyo hakustahiki yeye wala warathi wa Salum Omar kumrithi Omar Hassan Fatih, na hivyo kwa kuwa Wakata rufaa ni watoto wa baba mkubwa na mdogo wao ndio waliopaswa kumrithi Omar Hassan Fatih. Jambo hili lilipingwa na Mpinga Rufaa nam. 1 ambaye alisema kuwa Salum Omar Hassan ni mtoto halali wa Omar Hassan Fatih na amezaliwa ndani ya ndoa.

Kadhi wa Wilaya baada ya kusikiliza kesi hiyo alitoa hukumu tarehe 28.12.2020 na kusema:

> *"a) Mahkama inabatilisha Fatwa iliyotolewa na Afisi ya Mufti, Fatwa nam. 3 ya 2019 ya tarehe 27.2.2019*
>
> *b) Mahkama inafuta uamuzi uliotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" wa tarehe 8.6.2020 unaohusu mzozo wa shamba la marehemu Salum Omar Hassan la Fuoni Kipungani, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja.*
>
> *c) Mahkama inatamka kuwa marehemu Salum Omar Hassan sio mrithi wa marehemu Omar Hassan Fatih kwa mujibu wa Sheria ya mirathi katika uislamu.*

d) Mahkama inatamka kuwa familia ya Hassan Fatih Mohamed na Salama Fatih Mohamed ndio warithi halali wa marehemu Omar Hassan Fatih.

e) Mahkama inaamuru mdaiwa nam. 2, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana kuendelea na ugavi wa mirathi ya marehemu Omar Hassan Fatih kwa mujibu wa sharia za mirathi ya Kiislam.

f) Kila upande utabeba gharama zake."

Mpinga rufaa nam. 1 hakuridhika na uamuzi huo wa Kadhi wa Wilaya na hivyo kukata rufaa katika Mahakama ya Kadhi wa Rufaa. Rufaa hiyo ilisikilizwa na Naibu Kadhi Mkuu ambae baada ya kusikiliza rufaa hiyo alitoa hukumu yake tarehe 2.07.2021 ambapo aliitengua hukumu ya Kadhi wa Wilaya na kusema kwamba Salum Omar Hassan *alikuwa mtoto wa ndani ya ndoa. Hivyo, Kadhi wa rufaa alitoa amri zifuatazo:*

"a) Mahkama hii ya rufaa Vuga imeikubali rufaa hii.

b) Mahkama hii imetengua hukumu ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya kwenye kipengele a, b, c, na inaibakisha hukumu hiyo kwa kipengele (e + f)."

Wakata rufaa hawakuridhika na hukumu hiyo na wamekata rufaa katika Mahkama hii na wamewasilisha hati yao ya rufaa yenye sababu tatu za rufaa zinazofupishwa kama ifuatavyo:

1. Kwamba Sheikh Hassan Othman Ngwali, Kadhi wa rufaa alijielekeza vibaya kisomi, kiutendaji na kiuzoefu na alishindwa kuvikumbuka visaidizi vya kuamua jambo la kisheria (fact in issue, relevant fact, competency of the court, applicable law) na hivyo kudhani kwamba mzozo unahusu kutambuliwa marehemu Salum Omar Hassan Fatih kuwa ni mtoto wa nje ya ndoa au la, wakati mzozo haukuwa hivyo.
2. Kwamba ni hoja ya Wakata rufaa kwamba Kadhi wa rufaa alikosea kifikhi kwa kulipa uzito mkubwa fatwa yenye uhusiano tu iliyoibuka kwenye mjadala wa jambo lenyewe ambalo ni mirathi na kulipa uzito mdogo mzozo halisi na kutoa hukumu isiyowafikiana na ushahidi uliotolewa na kifungu cha 4 cha hati ya madai. Mzozo ni mirathi na si uzawa. Suala la uzawa linaweza kuamuliwa na

Mahkama Kuu pekee hivyo hukumu ya Kadhi wa rufaa ni batili na hukumu ya Kadhi wa Wilaya ndio sahihi.

3. Kwamba vyombo vyengine vilivyojadili suala hili pamoja na Kadhi wa rufaa walikosea katika maamuzi yao. Kadhi wa Wilaya ndie aliyekuwa sahihi.

Mahakama hii iliwasikiliza Wadaawa kuhusiana na rufaa hiIi. Kwa upande wa Wakata rufaa waliwakilishwa na Vakly Khamis Tamim, Mpinga Rufaa nam.1 alijiwakilisha mwenyewe na Mpinga rufaa nam. 2 aliwakilishwa na maafisa wa sharia, Assaa Jaffar na Haji Habib.

Vakly Khamis alianza kwa kueleza kwamba rufaa hii inahusu mirathi na wameleta sababu tatu za rufaa. Sababu ya 1 na 3 ya rufaa inajitosheleza yenyewe kimaelezo na alielezea sababu ya 2 ya rufaa. Alisema hoja kubwa katika madai yao inahusiana na mirathi lakini Kadhi wa Rufaa alikwenda kwenye uzawa. Nguzo tatu za mirathi zilitimia lakini Kadhi alisema mtoto Salum Omar Hassan ni mtoto wa ndani ya ndoa kitu ambacho wao wanakipinga. Katika mwenendo wa Mahkama ya Kadhi wa Wilaya katika ukurasa wa 7 Rajab (shahidi) alithibitisha kuwa Salum ni mtoto wa nje ya ndoa. Mama yake Salum aliolewa akiwa na mtoto anayetambaa. Aliendelea kueleza kuwa upande wa pili ulishindwa kuthibitisha kuwa Salum Omar ni mtoto wa ndani ya ndoa. Aliiomba Mahkama hii kubatilisha hukumu ya Kadhi wa Rufaa na kuyakubali maombi yao yaliyomo ndani ya hati ya rufaa.

Kwa upande wa Mpinga rufaa nam. 1, Salma alisema kuwa yeye ni mke wa mwanzo wa Salum Omar Hassan na mama wa marehemu Halima Salum Omar. Pia alieleza kwamba yeye amelelewa katika familia ya Fatih. Bi Salma aliendelea kueleza kwamba huwezi kuingia katika masuala ya mirathi bila ya kujua nasaba; na huwezi kumrithisha mtoto wa baba mdogo wakati mtoto wa halali yupo. Vile vile alisema mwenye haki ya kumkataa mtoto ni baba na ni ndani ya siku 7 baada ya kuzaliwa mtoto. Omar Hassan hakulifanya hilo.

Aliendelea kusema kwamba katika shauri hili hakuna mtu yoyote aliyethibitisha kuwa Salum ni mtoto wa nje ya ndoa kwa kauli ya baba yake. Wakata rufaa walilithibitisha hilo Mahkamani kuwa hawajawahi kumsikia Omar Hassan au wazee wengine katika familia. Shahidi Rajab pia hakulithibitisha hilo. Bi Salma alifafanua kwamba Mkata rufaa nam. 1 ameweza kumzika Salum baada ya kufa na kumuozesha Halima (mtoto wa Salum) katika ndoa ya kwanza na katika ndoa ya pili alimpa idhini mwanawe

amuozeshe na Halima alipokufa walimzika. Alisema kwamba sio kweli kwamba Mkata rufaa nam. 1 alipata idhini ya Kadhi kwani cheti cha ndoa kipo. Hivyo, kama Salum alizaliwa nje ya ndoa kwanini Mkata rufaa nam. 1 alikuwa walii wa mtoto wa Salum.

Vile vile alisema kwamba watoto wa Halima sasa hivi watafanywa nini ikiwa Halima aliozeshwa ndoa batili, yaani aliozeshwa na mtu ambae si walii wake. Pia Bi Salma alieleza kwamba Omar Hassan alikuwa akiishi Kisauni na Rajab alikuwa akiishi Kipungani, hivyo mambo aliyoyasema ni ya kusikia tu. Aliiomba Mahkama kulitizama suala hili kwa umakini kwani yeye amelelewa katika familia hiyo tokea akiwa na umri wa miaka 13 na hakuwahi kusikia kuwa Salum ni mtoto wa nje ya ndoa.

Mwakilishi wa Mpinga rufaa nam. 2, Assaa Jaffar alieleza kwamba mzozo huu ni kuhusu Salum Omar Hassan je ni mrithi wa marehemu Omar Hassan Fatih au la. Alisema katika mzozo kama huu wao hawatoi ushahidi; ushahidi unatolewa na wadaawa wenyewe kwa kueleza juu ya nasaba. Wao wanasubiri maelekezo tu.

Vakly Tamim katika maelezo yake ya ziada alikubali kwamba Hassan Fatih hakuweza kuthibitisha jambo hilo lakini shahidi Rajab ameshuhudia tukio hilo.

Tukianza na sababu ya 1 na ya 3 ya rufaa ambayo imemlalamikia Kadhi wa Rufaa kuwa hakuuelewa mzozo uliopo Mahkamani na ameliamua suala jengine. Kama tulivyoeleza awali kwamba kesi iliopelekwa Mahkamani ni kesi ya mirathi, lakini mzozo hasa wenye kuamua mirathi hiyo ni juu ya suala la je Salum Omar Hassan ni mtoto halali wa marehemu Omar Hassan Fatih. Ingawa Kadhi wa Rufaa hakutaja kwamba hiyo ilikuwa ni kesi ya mirathi lakini aliufahamu vyema mzozo uliopo mbele yake na katika ukurasa wa 1 wa hukumu alisema:

> *"Rufaa hii inahusu dai la kutambuliwa kwa marehemu Salum Omar Hassan ni mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa ya marehemu Omar Hassan Fatih au amezaliwa nje ya ndoa."*

Hivyo, kutotaja suala la mirathi hakukuathiri maamuzi kwenye suala hilo kwani katika amri zake alikubaliana na Kadhi wa Wilaya kuwa Mpinga rufaa nam. 2 aendelee na ugavi wa mirathi. Hivyo, sababu ya 1 na 3 za rufaa hazina msingi wowote na zinatupiliwa mbali.

Kuhusiana na sababu ya 2 ya rufaa Vakyl wa Wakata rufaa alikubali kuwa Wakata rufaa wenyewe pamoja na mashahidi wao hakuna aliyekuwa na ithibati kwamba Salum Omar Hassan alikuwa mtoto wa nje ya ndoa. Vile vile hakuna hata mmoja aliyewahi kushuhudia Omar Hassan Fatih akimkana Salum Omar kuwa si mwanawe au hata kumsikia akisema kuwa si mwanawe. Wao waliegemea ushahidi uliotolewa na Rajab Fatih Fum uliopo katika ukurasa wa 7 wa mwenendo wa kesi ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya ambaye alisema kwamba: Omar Hassan Fatih alioa mwanamke ambae tayari alikuwa na mtoto anaetambaa. Lakini shahidi huyu aliendelea kueleza kwamba yeye hakuwahi kuambiwa na Omar Hassan Fatih kwamba Salum ni mtoto wake wa nje ya ndoa. Vile vile kauli ya shahidi huyu hakuwahi kuizungumza kabla ya kuja hapa Mahkamani na inaelekea kwamba kutokana na ushahidi huu ndipo Kadhi wa Wilaya akaamua kwamba Salum Omar Hassan ni mtoto wa nje ya ndoa.

Mahkama hii inakubaliana na Kadhi wa Rufaa kwamba Kadhi wa Wilaya alikosea kwenye maamuzi yake kwani ushahidi wa aina hii ulipaswa kuthibitishwa na mashahidi wawili; lakini Wakata Rufaa wameleta shahidi mmoja tu kuthibitisha hilo. Vile vile ushahidi huu umekuja baada ya miaka 40 baada ya baba Omar Hassan Fatih kufariki 1980. Hivyo, ushahidi huo hauna nguvu.

Kuhusiana na suala la kukataa nasaba suala hili ni zito sana na ni vyema kubakia katika asili kwa vile ndoa ilikuwepo. Allah (S.W.T) katika aya ya 5 ya Suratul Ahzab amesema:

> *"Waiteni kwa (ubini wa) baba zao, maana huo ndio uadilifu mbele ya Mwenyezi Mungu" (33:5, Tafsiri ya Sk. Abdalla Saleh Farsy)*

Nae Dr. Abdulkareem Ziidan katika kitabu cha **Al-Mufaswal fii ahkamil mar'at wa baitil Muslim**, chapa ya 3 ya mwaka 2000, mjeledi wa 9 ukurasa wa 315 akielezea maelezo ya Imaam Al Qurtubi kuhusiana na aya niliyoinukuu hapo juu ameeleza:

> "Lililo bora na lazima na uadilifu zaidi ni kunasibishwa mtu kwa baba yake"

Vile vile katika ukurasa wa 316 mpaka 317 wa kitabu hicho katika kanuni za nasaba Dr. Abdulkareem ameeleza yafuatayo.

“Tumesema kuwa hakika katika nasaba kuna haki ya Mwenyezi Mungu na kuna haki ya mtoto, kwa hiyo mtu yoyote hamiliki kukana nasaba ya mtoto baada ya kuthibiti kwake…, na vile vile hamiliki mtu yoyote kukana nasaba ya kilichozaliwa kutokana na yeye isipokuwa kwa masharti waliyoelezea maulamaa katika suala la “liaan”- kulaaniana mke na mume…”

Pia Sk. Mohamed Mustafaa Al Zuhaily katika kitabu cha Fiqhi, mjeledi wa 1, ukurasa wa 129 kanuni ya 3 inasema.

“Asili ya kitu ni kubakia kilichokuwa kama kilivyokuwa“

Hivyo, jambo lolote au hukumu ambayo imethibiti katika wakati uliopita ima kwa kukubalika au kukataliwa basi itabaki katika hali yake na wala haitobadilika ikiwa hakuna hoja ya kubadilisha. Pia msingi na kipimo katika mambo yaliyokuja mwishoni ni kuwa yajengewe kutokana na mambo yaliyotangulia, na ikiwa haikujulikana wakati wa mgogoro hali ya jambo na wala hakuna hukumu yoyote inayohukumu kwa muktadha wake, na ikiwa jambo hilo lina hali iloyozoeleka na imetangulia tokea mwanzo, basi asili katika hilo ni kuhukumiwa kubakia na kuendelea na hali iliyozoeleka ambayo ndio ilikuwapo tokea mwanzo.

Kuhusu masharti ya kukana mtoto ni kuwa haki hiyo ni ya baba, na katika masharti ya kukana ni kuwa asicheleweshe kukana mtoto. Kwa hivyo, nasaba inathibiti na zinathibiti haki nyengine zinazofungamana na haki hiyo, ikiwemo mirathi, nk.

Kwa hivyo, kwa ujumla wa tuliyoyaeleza ni kwamba hakuna mwenye haki ya kukana nasaba ya mtoto baada ya kuwa baba yake mpaka amefariki hakuwa amemkana mwanae tokea kuzaliwa hadi kufariki kwake; na vile vile ikiwa hakuna ushahidi wowote unaothibitisha kuwa mtoto si wa baba mtajwa na wala baba hakuacha wasia wa aina yoyote juu ya hilo. Na pia hata katika hali ya kuwepo shubha ya ndoa basi mtoto hunasibishwa kwa baba yake.

Katika kesi hii marehemu Omar Hassan Fatih hakuwahi katika uhai wake kumkana mtoto huyo au kusema ni mtoto wa nje ya ndoa, na mpaka Omar Hassan Fatih anafariki hakuna aliyewahi kusema jambo hilio. Vile vile alipofariki Salum Omar upande wa ubabani yaani upande wa Omar Hassan Fatih ulipata nguvu na kumzika Salum Omar. Pia mtoto wa Salum Omar, Halima aliozeshwa na familia ya Omar

Hassan Fatih na alipofariki wao ndio waliomzika. Hivyo, hii ndio hali ilivyokuwa na ndio inavyotakiwa kubakia.

Hivyo, Mahakama inaikataa rufaa hii na inaunga mkono hukumu ya Kadhi wa Rufaa na inatamka kwamba Salum Omar Hassan ni mtoto halali wa Omar Hassan Fatih na warathi wanaotokana na Salum Omar wanayohaki ya kurithi shamba lililopo Fuoni Kipungani. Mpinga rufaa nam. 2 anaamriwa kuendelea na mirathi kwa kuwarithisha warithi mali za Omar Hassan Fatih kama taratibu zinavyotaka. Kila upande utabeba gharama zake za kesi.

Hii ni hukumu iliyotolewa na Mahkama hii.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa Jaji

26/1/2023

(Imes.)

Sk. Sameer Zulfikar

Imes.)

Sk. Saleh Hakim

(Imes.)

Sk. Juma Fakih

(Imes.)

Sk. Kani Mkanga

MAHKAMA

Hukumu hii imesomwa leo tarehe 26/1/2023 mbele ya Mkata rufaa na Mpinga rufaa nam. 1, na mbele ya mwakilishi wa Mpinga rufaa nam. 2, Bw. Hassan Nassor.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa Jaji

26/1/2023

Nathibitisha kwamba hii ni nakala halisi ya hukumu

……..

MRAJIS

MAHKAMA KUU, ZANZIBAR